



P.O. Box 11372
Mt. Meru Post Office
Arusha, Tanzania
info@ccr-tz.org
www.ccr-tz.org

Taarifa kwa Vyombo vya Habari
27 Novemba 2009,

Tunaweza kuadhimisha miaka 20 ya Haki za Mtoto na Sheria Mpya ya Watoto, lakini bado tuna safari ndefu kabla ya kuona matokeo katika kuwalinda watoto wa Tanzania.

Ni kwa masikitiko makubwa kwamba Caucus for Children's Rights inapitia changamoto ambazo Tanzania hukabiliana nazo katika kuleta uhalisia wa haki za mtoto. Siku ambayo ulimwengu mzima ulisherehekea Maadhimisho ya Miaka 20 ya Mapatano ya Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Mtoto tulikuwepo Mahakama Kuu ya Tanzania kusikiliza hukumu ya kesi ambayo imedumu kwa muda mrefu juu ya ufutwaji wa sheria ya Mamlaka ya Manispaa ambayo inaendeleza misako (kamatakamata) na kuwaweka kizuizini watoto wa mitaani.

Mwaka 2007, Wanachama wa Caucus for Children's Rights walifungua kesi ya Ki-katiba wakitoa hoja za msingi juu ya kufutwa kwa Sheria za Miji (Kuondolewa kwa Watu Wasiofaa), Sheria ya Watu Fukara, na Azimio kwamba kifungu cha 14(h) na 28(b) cha Sheria ya Makosa ya Jinai na vifungu vya 176(2) na 177 vya Kanuni ya Adhabu viko kinyume na Katiba hivyo havina nguvu kisheria. Hili lilikuwa jaribio la kuleta ukomo wa mazoea ya muda mrefu (kiutendaji) ya Manispaa nyingi hapa Tanzania kuwakamata watoto wa mitaani, kwa madai kwamba hao watoto **hawatakiwi kuonekana maeneo hayo**. Wanachama hawa wa Caucus walidai kwamba sheria na hizo kamatakamata zinapingana na Ibara ya 15 ya Katiba Ya Tanzania, kwa kuwa zinaruhusu kuwatia watoto mbaroni, kuwekwa kizuizini au kuwanyima uhuru wao, tena haina kusudio la maana. Pia walidai kwamba mwikitiko huu wa Watoto wa Mitaani hauwiani, hauna mantiki, holela na usio na ulinzi/utaratibu tetezi wa kutosha kikanuni. Sheria ya Miji (Kuondolewa kwa Watu Wasiofaa) na Sheria ya Watu Fukara, zote mbili ziko kinyume na Ibara ya 17 ya Katiba, kwamba zinaingilia haki za raia wa Tanzania kwenda na kuishi popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwisho, sheria zote nne ziko kinyume na Ibara ya 12 na 13 ya Katiba, kwa kuwa (i) zinashindwa kuwatofautisha watoto na watu wazima na (ii) kuwatofautisha watoto wa Mitaani na watoto wengine. Huu ni ubaguzi wa haki na kisheria na kinyume cha kanuni ya usawa.

Hii kesi imekuwa ikisikilizwa takriban miaka miwili na wakati huo kanuni ya maslahi bora ya mtoto na haki zao za kuishi bila kubaguliwa zimeandikwa katika Sheria Mpya (ya Tanzania) ya Mtoto. Hata hivyo, hukumu hii



**Half of Tanzania's population is under the age of 18. The FUTURE is NOW.
Learn more and join the 50% Campaign to Protect Children: www.50campaign.org**

inaonesha bado tuna safari ndefu mno kabla ya kufikia kuhakikisha kwamba maslahi bora ya mtoto yanalindwa na kudumishwa. Kwa umakini kabisa, majaji walitetea manufaa ya umma ambayo ni kulinda miji na manispaa kusiwe na watu wasiotakiwa, fukara na wazembe. Vivyo hivyo kwamba ilikuwa ni kwa manufaa ya umma kuwachukulia watu kama wahalifu kulingana na hali duni na umaskini wao. Pia walitetea kwamba si kwa manufaa ya umma kuwachukulia watoto tofauti na watu wazima. Matokeo yake ni kwamba bado sheria hii inaruhusu kumweka kizuizini mtoto yeyote aliye mtaani kiholela bila uangalizi wa mtu mzima.

The Caucus for Children's Rights inakusudia kukata rufaa kwa kupinga uamuzi huo wa mahakama.

Kwa Maelezo Zaidi:

Francis Kiwanga: Email: fkiwanga@humanrights.or.tz +255 787229933

Kate McAlpine: Email: info@ccr-tz.org +255 787 603334